East African Journal of Swahili Studies, Volume 5, Issue 2, 2022
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1019

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 5, Issue 2, 2022
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Utathmini wa Ujenzi wa Motifu ya Mgogoro wa Ardhi Kupitia Wahusika: Mfano Kutoka Chozi la Heri na Kovu Moyoni

*Mercy Karimi Nthia[1*] & Dkt. Onesmus Gitonga Ntiba, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Mlima Kenya, S. L. P. 109¬-60400, Thika, Kenya.
[*] ORCID ID https://orcid.org/0000-0001-9300-4622; Barua pepe ya mawasiliano: zabkarimi@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1019**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*22 Desemba 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Ardhi, Migogoro, Motifu, Uhalisia na Wahusika.*

**IKISIRI**

Suala la ardhi limekuwa nyeti tangu jadi. Wahusika hutumiwa na wasanii kubainisha suala hili. Tafiti za awali zilijikita katika motifu ya safari, siri na maisha ya dunia. Hata hivyo, hakuna utafiti umefanywa kutathmini ujenzi wa motifu ya mgogoro wa ardhi kupitia wahusika. Makala hii imelenga kuziba pengo hili. Utafiti huu ni kutathmini ujenzi wa motifu ya suala la mgogoro wa ardhi kupitia wahusika; mfano kutoka *Chozi la Heri* na *Kovu Moyoni*. Motifu hii ni kurudiwarudiwa kwa suala la mgogoro wa ardhi baina ya wahusika katika matini teule. Makala hii iliongozwa na nadharia mbili; Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa na Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi. Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa iliwaongoza watafiti kuweza kubainisha suala la ardhi kama lilivyoangaziwa na waandishi katika uhalisia wake. Hata hivyo, nadharia hii ilipungukiwa kubainisha jinsi matabaka katika jamii huendeleza suala la ardhi. Nadharia iliyofidia pengo hili ni Sosholojia ya Fasihi. Utafiti huu ulikuwa wa maktabani ambapo matini teule ziliteuliwa kimaksudi. Mpango wa kimaelezo ulitumika kuchanganua na kuwasilisha matokeo. Matokeo ya makala hii ni kuwa motifu ya mgogoro wa ardhi imekuzwa kupitia kwa wahusika antagonisti, protagonisti, tuli na bui. Kwa hivyo, utachangia katika uhakiki wa kazi za baadaye za nathari za fasihi ya Kiswahili. Aidha, walimu na wanafunzi wataelewa namna wahusika hujengwa. Makala hii ilipendekeza tafiti za baadaye zifanywe kutathmini motifu ya wahusika katika sekta ya uchumi na siasa.

**APA CITATION**

Nthia, M. K., & Ntiba, O. G. (2022). Utathmini wa Ujenzi wa Motifu ya Mgogoro wa Ardhi Kupitia Wahusika: Mfano Kutoka Chozi la Heri na Kovu Moyoni. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(2), 142-154. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1019.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

**CHICAGO CITATION**

Nthia, Mercy Karimi and Onesmus Gitonga Ntiba. 2022. "Utathmini wa Ujenzi wa Motifu ya Mgogoro wa Ardhi Kupitia Wahusika: Mfano Kutoka Chozi la Heri na Kovu Moyoni". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (2), 142-154. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1019.

**HARVARD CITATION**

Nthia, M. K., & Ntiba, O. G. (2022) "Utathmini wa Ujenzi wa Motifu ya Mgogoro wa Ardhi Kupitia Wahusika: Mfano Kutoka Chozi la Heri na Kovu Moyoni", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(2), pp. 142-154. doi: 10.37284/jammk.5.2.1019.

**IEEE CITATION**

M. K. Nthia, & O. G. Ntiba "Utathmini wa Ujenzi wa Motifu ya Mgogoro wa Ardhi Kupitia Wahusika: Mfano Kutoka Chozi la Heri na Kovu Moyoni", *EAJSS*, vol. 5, no. 2, pp. 142-154, Dec. 2022.

**MLA CITATION**

Nthia, Mercy Karimi & Onesmus Gitonga Ntiba. "Utathmini wa Ujenzi wa Motifu ya Mgogoro wa Ardhi Kupitia Wahusika: Mfano Kutoka Chozi la Heri na Kovu Moyoni". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 2, Dec. 2022, pp. 142-154, doi:10.37284/jammk.5.2.1019.

## UTANGULIZI

Baadhi ya vipengele tajika katika kazi za fasihi ni mgogoro. Migogoro ni nyenzo kuu ambayo huendeleza kazi yoyote ya fasihi na kuipa fursa ya kuwekwa katika kategoria ya kazi bora au chapwa. Kwa mujibu wa Scott (2015), migogoro ni misuguano, mikinzano au kutoelewana kwa pande mbili au zaidi katika kazi za fasihi. Migogoro ya aina mbalimbali inaweza kupatikana katika kazi za fasihi ambayo huelekeza mtiririko wa vitushi katika kazi hiyo.

Makala hii ililenga kuangazia wahusika katika ujenzi wa motifu ya mgogoro wa ardhi katika riwaya teule. Motifu ni kipengele cha kijadi kinachohusu kurudiwarudiwa kwa wazo au dhamira fulani katika sehemu kubwa ya kazi za fasihi hususani riwaya, tamthilia, ushairi na fasihi simulizi (Mulokozi, 1996). Kurudiwarudiwa kwa suala la ardhi katika riwaya teule na kuwasilishwa kupitia kwa wahusika mahususi kulikuza uhalisia ambao watunzi walitaka wasomaji kuupata. Suala la migogoro ya ardhi ni baadhi ya motifu zinazokuzwa katika riwaya teule. Hii ni kwa sababu motifu ni kazi inayotawala kazi ya fasihi na huwa ni sehemu ya wazo kuu la mwandishi (Cuddon, 2013).

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), migogoro ni mivutano inayokuwa kati ya mhusika mmoja na mwingine katika kazi ya fasihi au kati ya mhusika mmoja na mwingine katika kazi ya fasihi au katika akili ya mhusika mmoja na huchukua sehemu kubwa ya usimulizi wowote ule wa fasihi. Migogoro hii inaweza kutokea katika kiwango cha mhusika fulani na nguvu fulani au mhusika mwingine. Utafiti huu ulijikita kwenye mgogoro kuhusu suala la ardhi baina ya mhusika na mhusika mwingine au jamii kwa jumla katika riwaya ya *Chozi la Heri* na *Kovu Moyoni*.

## MWAUO WA MAANDISHI

Ardhi huwapa wanadamu mahali pa kulala, maji, chakula.Suala la mgogoro wa ardhi ni nyeti katika ulimwengu na kwamba limekita mizizi tangu jadi na kuathiri maendeleo katika nyanja nyingi ulimwenguni (Zhang na wengine,2007). Maelezo haya yanasaidia kwa kubainisha ardhi kama chombo muhimu katika kuendeleza maisha ya binadamu. Tofauti iliopo ni kwamba maelezo haya yameangazia uhalisia wa maisha lakini utafiti huu umelenga kuangazia kazi za kibunilizi ukijikita katika Uhalisia wa wahusika katika mgogoro wa ardhi katika riwaya teule.

Gyamera na wengine (2018), walitafiti kuhusu chanzo na suluhisho la migogoro ya ardhi nchini Ghana. Utafiti wao ulibainisha kuwa baadhi ya mila za Waghana haswa matumizi ya mawe na mito kubaini mipaka ya ardhi huzua migogoro ya ardhi. Mipaka hii baada ya muda hupotea na hivyo kufanya wahusika wa mashamba yanayopakana kuchanganyikiwa pale mashamba yao yameanzia na kufika tamati. Mawazo haya yanaufaa utafiti huu kwa kubainisha kuwa baadhi ya mila zinazozingira ardhi haswa mipaka ya ardhi huzua migogoro ya ardhi. Utafiti wake ulifaa utafiti huu katika kueleza namna michakato mbalimbali ya jadi iliendeleza mizozo ya ardhi katika jamii ya sasa.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1019

Wizara ya Ardhi nchini Kenya (2009), inabainisha kuwa Kenya ilipopata uhuru wake, ilitarajiwa kwamba matatizo ya ardhi yangelitatuliwa kwa kuunda sera tofauti na zile zilizobuniwa na Wakoloni. Hakuna mikakati iliyobuniwa, badala yake, serikali zilizoridhi utawala huo ziliendelea kutumia sheria hizo za ardhi za wakoloni naye rais na tume ya ardhi kutumia nguvu kumiliki ardhi nchini. Hatua iliyosababisha mwenendo wa unyakuzi wa ardhi, na ongezeko la uhasama na chuki baina ya maskini na makundi yaliyotengwa kutokana na uhasama wa kisiasa. Madai haya yanaufaa utafiti kwani yanabainisha kichocheo na athari za migogoro ya ardhi ambayo ndiyo ilibainika katika utafiti huu. Tofauti iliyopo ni kwamba wizara ya ardhi inaangazia uhalisia wa jamii ya Kenya katika kipindi cha ukoloni lakini utafiti huu unaangazia fasihi bunilizi katika riwaya za *Chozi la Heri* na *Kovu Moyoni*.

## MISINGI YA NADHARIA

Uhalisia wa Kijamaa na Sosholojia ya Fasihi ni nadharia ziliteuliwa na kukamilishana katika kuongoza mtafiti kuyafikia malengo ya utafiti. Nadharia ya Uhalisia ni mkondo unaosisitiza usanii wa matukio au maisha katika fasihi kama yalivyo katika maisha ya kila siku.

Baadhi ya mihimili ya nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa iliyotumiwa ni pamoja na; Wahusika katika sanaa ya kihalisia husawiriwa wakiwa wa kawaida na wakiwakilisha jamii zao, lugha katika kazi za kihalisia huwa ya kawaida na wahusika wanaitumia kama ilivyo katika hali halisi ya ulimwengu, mandhari na matukio yanafaa kuwa yale yanayowezekana na msanii huangalia matatizo ya jamii na kuchunguza chanzo chake. Nadharia ya uhalisia wa kijamaa ilipungukiwa kufafanua jinsi sanaa haswa riwaya huonyesha miundo ya kijamii kama vile matabaka yanavyozua migogoro na mivutano baina ya wahusika katika jamii. Upungufu wa nadharia hii ulipelekea kutafuta nadharia ya Sosholojia ya Fasihi iliofidia pengo hili.

Nadharia ya Sosholojia ya fasihi iliasisiwa na Georg Lukacs, mwanaitifaki wa Karl Marx (Wien, 1916) wa Ujerumani. Nadharia hii ilitumika ili kuongoza katika kutathmini uhusiano uliopo baina ya masuala ya kijamii kama vile migogoro ya ardhi na kazi za kifasihi hasa riwaya za *Chozi la Heri* na *Kovu Moyoni*. Mihimili ya nadharia ya Sosholojia ya Fasihi iliyosaidia katika Makala hii ni; Kazi ya Sanaa hasa riwaya inapaswa kuonyesha miundo ya kijamii na ukamilifu wa maisha kwa kuangaza mivutano na mikinzano au migogoro iliyopo, Jinsi mwandishi alivyoandika kazi yake ya Sanaa hutegemea kipindi alichoandika na kazi ya sanaa inataathira kwa wanajamii.

## MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulitumia mpango wa kimaelezo katika kuchanganua data na kuwasilisha matokeo ya utafiti.Riwaya za *Chozi la Heri* na *Kovu Moyoni* ziliteuliwa kimakusudi ili kupata data. Mugenda na Mugenda (1999), wanasema kuwa katika mbinu ya kimakusudi, watafiti huwa na uhuru wa kuteua sampuli zilizo na data iliyohitajika. Matini teule zilisomwa na data iliyokusanywa kuchanganuliwa kimaelezo. Data hiyo iliegemea katika matumizi ya motifu ya mgogoro wa ardhi.

Utafiti huu ulijikita maktabani na kudengua matumizi ya motifu ya migogoro ya ardhi katika kazi teule. Data iliyopatikana ilichanganuliwa kwa njia ya kimaelezo kwa kuongozwa na madhumuni ya utafiti. Uchanganuzi huo uliongozwa na uhalisia ili kueleza namna ambavyo waandishi wa kazi teule wameifanikisha dhamira yao ya kujenga motifu migogoro ya ardhi kupitia kwa wahusika.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Wahusika katika Motifu ya Mgogoro wa Ardhi

Lengo la utafiti huu ni kuchunguza jinsi wahusika walivyoendeleza ujenzi wa motifu ya suala la migogoro ya ardhi katika kazi teule.Makala hii ilibainisha wahusika protagonisti, antagonisti, tuli na bui na jinsi walivyoendeleza motifu ya mgogoro wa ardhi katika riwaya teule.

#### *Protagonisti katika Riwaya ya Chozi la Heri*

Protagonisti ni mhusika mkuu katika kazi ya fasihi (Saraswati, 2019). Ni wahusika duara ambao mara nyingi huibua hisia za huruma kwa msomaji wa kazi bunilizi. Kazi yoyote ya fasihi haiwezi kuendelezwa bila kuwepo kwa wahusika protagonisti. Hata hivyo, wahusika hawa wanaweza kuwa na hulka chanya au hasi. Ni muhimu kuhusisha wahusika hawa na hai halisi za maisha ili hulka yao iwasilishe

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1019

wazo kamili la mwandishi. García (2016) anaeleza kuwa ni muhimu kwa wasomaji kuamini na kuelewa uamuzi wa protagonisti ili waelewe kazi yoyote ya fasihi. Wamitila (2002), anasisitiza kuwa mhusika protagonisti huwa 'midomo' ya wasanii. Mwandishi amebainisha mhusika Ridhaa kuwa Protagonisti katika riwaya ya *Chozi la Heri*. Anaendeleza motifu ya mgogoro wa ardhi kwa njia nyingi.

Kwanza, kuna nyumba ilichomwa. Jirani yake Ridhaa , Mzee Kedi alichoma nyumba ya Ridhaa na kumwangamizia aila yake. Hali hii inaletwa na uhasama unaoibuka kati yao baada ya uchaguzi mkuu ambapo wenyeji walianza kuwafukuza wageni. Kitendo hiki kinaangamiza Terry – mkewe Ridhaa, Tila – mwanawe Ridhaa na mjukuu wake Becky. Mwandishi anasema:

> *Sasa Ridhaa anatazamana na majivu ambayo bila shaka ni miili ya wanawe wawili, mkewe, mkaza mwanawe na mjukuu wake, Becky. Anawaona wote mbele ya macho yake yaliojaa mavune (Uk. 5).*

Aidha, Terry, mkewe Ridhaa aliweza kumtambua Mzee Kedi na kumwomba asiwateketeze lakini Mzee Kedi alipuuza ombi lake. Haya yanadhibitishwa na kifungu kifuatacho:

> *"Uuuui! Uuuui! Jamani tusaidieni! Uuuui! Uuuui! Mzee Kedi, usituue, sisi tu majirani! Maskini wanangu! Maskini mume wangu!"* (Uk. 3).

Nyiri (2014) anasema kuwa machafuko yaliyoshuhudiwa nchini Kenya baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2007 yalichochewa na uhasama wa kikabila haswa kati ya jamii ya Wakalenjini na Wamasai dhidi ya Wakikuyu. Matei anaonyesha vile Mzee Kedi alivyoiangamiza familia ya Ridhaa kwa sababu ya uhasama uliozuka baina yao baada ya uchaguzi mkuu katika nchi ya Wahafidhina.

Pili, kuna nyumba zilibomolewa. Wizara ya Ardhi na Makao ikishirikiana na Wizara ya Uchukuzi na Mawasiliano zinayabomoa majumba ya Ridhaa. Madai ya Wizara hizi ni kuwa majumba haya yalikuwa yamejengwa mahali ambapo palitengwa kwa ujenzi wa barabara na vigingi vya nyaya za stima. Mwandishi anasema:

> *Matrekta ya Baraza la jiji yamefanya kazi ya Waheshimiwa alasiri ya leo… matrekta hayo yalizibomoa nyumba ishirini katika mtaa wa Tononokeni. Ilidaiwa kuwa majumba haya yalikuwa yamejengwa mahali ambapo pametengewa kwa ujenzi wa barabara. Mengine yalikuwa yamejengwa chini ya vigingi vya stima* (Uk. 13).

Kitendo hiki kinamfanya Ridhaa kuyapoteza majumba yake matano. Hali hii inamwathiri kisaikolojia na kiuchumi kutokana na hasara anayopata. Mwandishi anasema:

> *Ridhaa alitazama picha za manyumba yake matatu kwenye runinga …manyumba haya sasa yamegeuka udongo… Anayatazama mengine mawili ambayo akili yake haitaki kukumbuka* (Uk. 13).

Mojawapo wa matokeo ya vita kuhusu suala la ardhi ni kuharibu mali yakiwemo majumba. Haya yanadhibitishwa na mwandishi wa riwaya ya Chozi la Heri anapoonyesha jinsi majumba ya Ridhaa yalivyobomolewa kwa madai kuwa yalikuwa yamejengwa sehemu ambazo serikali ilikuwa ijenge barabara na kuwa mengine yalikuwa chini ya vigingi vya stima. Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa migogoro ya ardhi baina ya wahusika huleta madhara mengi ambayo huchangia kuzorotesha uchumi kwa kulemaza maendeleo ya jamii.

Tatu,wahusika hutoa ushauri wa suala la mgogoro wa ardhi. Ridhaa anamshauri Mwangeka kufanya uchunguzi kuhusiana na kiwanja alichokuwa anataka kununua na kuanza ujenzi wa nyumba yake. Anamwonyesha hatari iliyopo dhidi ya utapeli wa mashamba siku hizi. Haya yanadhibitishwa na kifungu kifuacho:

> *Baba yake alimtahadharisha dhidi ya kuanza ujenzi kabla ya uchunguzi kufanywa kuhusiana na kiwanja chenyewe. Siku hizo masuala kuhusu umiliki wa ardhi hayakupigwa darubini kama ilivyo sasa* (Uk. 57).

Ridhaa anampa mwanawe ushauri kuhusu kufanya uchunguzi wa kipande cha ardhi ili asije akatapeliwa katika ununuzi wa kiwanja. Anamwongoza pia katika kutilia maanani umiliki wa kile kipande asije akapewa hatimiliki bandia na

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1019

hatimaye kufukuzwa pale. Kwa mujibu wa katiba ya Uganda (1995) sura ya 15, mada ya ardhi na mazingira ya nchi ya Uganda yameelezwa. Waganda wanaweza kumiliki ardhi kwa njia zilizoidhinishwa na katiba, mwongozo unaosaidia jamii kusuluhisha migogoro ya ardhi kama inavyobainishwa na waandishi wa riwaya teule. Kutokana na maelezo haya, ardhi huwa na mikakati ya kufuatiwa ili mja aweze kuimiliki. Kwa hivyo, ni bora wanajamii kuzingatia mikakati hii ili wasije wakajuta baadaye na kuzua migogoro ya ardhi.

Nne, mabomba ya kuhifadhi maji yalijengwa. Ridhaa anajenga maboma ya kuhifadhi maji katika eneo alilouziwa na kuishi na familia yake. Alichangia katika kubadilisha mazingira ambayo awali yalikuwa jangwa na kuwa ardhi yenye rutuba. Maboma haya pia yaliweza kuwapa wanajamii maji ya kutumia nyumbani na mashambani.

> *Mimi binafsi nimefanya juu chini, kuhakikisha kijiji kizima kimepata maji ya mabomba. Eneo ambalo awali likiitwa Kalahari sasa limetwaa rangi ya chanikwiti. Mibambakofi, mivule na miti mingine mingi imepandwa. Mvua inayesha majira baada ya mengine* (Uk.12).

Mwandishi anatuonyesha mchango wa Ridhaa katika kubadilisha ardhi ambayo ilikuwa jangwa hadi kuwa ardhi yenye manufaa kwa wanajamii. Ridhaa aliweza kuyajenga mabomba ya kuhifadhi maji wanajamii wakaweza kupata maji ya kutumia nyumbani na hata mashambani. Mazingira yalibadilika kutoka jangwa na kuwa na rangi ya kichanikiwiti kutoka na mchango huo.

Tano, kuna wahusika hushiriki katika mijadala inayohusu migogoro ya ardhi. Ridhaa anajadiliana na bintiye Tila kuhusu migogoro ya ardhi katika sehemu kame kwa ukosefu wa maji katika eneo lile. Katika mjadala huu, Ridhaa anamfafanulia Tila njia ambazo watu wanaoishi katika sehemu kame wanapaswa kutumia ili kuwa na maji ya kuimarisha mazingira yao. Anaonyesha umuhimu wa vijana kujitolea kwa kuchimba mabomba ili kuwa na maji ya kutosha. Mwandishi anasema:

> *Basi watumie maji ya mabomba! Si lazima wahifadhi ya mvua!... Vijana hawapaswi kungojea kufanyiwa kila kitu. Tumewapa nyavu, nao wanaona wangoje kuletewa samaki* (Uk. 43).

Aidha Ridhaa anamfafanulia Tila mchango wa serikali katika kukuza motifu ya mgogoro wa ardhi. Anamweleza kuwa serikali ina mpango wa kusambaza maji na umeme katika sehemu za mashambani hususani ili kupunguza migogoro ya ardhi iletwayo na ukosefu wa maji.

> *Serikali imeanzisha mpango wa kusambaza huduma za maji na umeme katika sehemu za mashambani, hususan zile kame. Wanachohitaji ni subira tu* (Uk. 44).

Matei anaeleza ushirikiaji katika mijadala ya migogoro ya ardhi anapoonyesha mjadala wake Ridhaa na Bintiye. Mjadala huu unaonyesha jinsi wanajamii hutegemea mvua katika kilimo chao na hatimaye kulalamika isiponyesha na mavuno yao kupungua. Aidha, anaonyesha jinsi serikali husaidia kuimarisha na kupunguza migogoro ya ardhi kwa kuweka mipango ya kuboresha ardhi haswa katika sehemu kame.

Morgan (1995), alifafanua hali ya maji katika sehemu kame. Utafiti wake ulibainisha kuwa serikali ya Misri imejitolea kuhakikisha kuwa Wamisri wamepata maji safi sio tu kwa kipindi kifupi bali milele, hali inayoelezwa na Ridhaa kwa Tila. Kutokana na maelezo haya, serikali ya nchi yoyote ina uwezo wa kuamua hali ya mazingira. Inaweza kubadilisha jangwa kwa kuitia rutuba na maji na ardhi ikawa ya manufaa kwa wanajamii na hivyo kuboresha uchumi wa nchi.

Sita, kuna wahusika huhama kutoka shamba lao la asilia. Baba yake Ridhaa, Mzee Mumo Msubili anawahamisha wake wake wa mwisho Ughaishuni kutokana na wingi wa vinywa katika familia yake ikilinganishwa na shamba ndogo alilomiliki. Ridhaa ana bahatika kuhama kwani alikuwa mmoja kati ya wana wa wake wale wawili waliohamishwa.

> *Wingi wa vinywa vya kulishwa ulizua uhasama, migogoro na uhitaji mkubwa. Mzee Mwimo akaona ku moto, akaamua kuwahamishia wake wawili wa mwisho Msitu wa Heri au Ughaishu, kama walivyouita watu wa huko… Ridhaa aliangukiwa na bahati kwani mama yake ndiye aliyekuwa mke wa mwisho* (Uk. 9).

Mwandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri* anaonyesha jinsi Mzee Mwimo Msubili alivyoweza kuhamisha wake wawili baada ya familia yake kuwa kubwa na

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1019

migogoro mingi ya ardhi kuzuka kutokana na wingi wa vinywa vya kulishwa ikilinganishwa na shamba lake lililokuwa lidogo.

Maelezo haya yanaonyesha umuhimu wa ardhi sio tu kwa kizazi cha sasa bali hata kwa vizazi vijavyo. Umuhimu wa rasilmali hii huridhishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Maelezo haya pia yanaonyesha umuhimu wa kupanga uzazi ili kuwa na idadi ya watoto ambayo inaweza kupata ardhi ya kutosha, jambo litakalopunguza migogoro ya ardhi katika jamii.

Saba,Ridhaa anaenda kuishi katika mtaa wa Afueni. Hatimaye Ridhaa anahamia katika jumba lake la kifahari katika mtaa wa Afueni. Anamweleza Mwangeka kwamba anahisi kuwa muda wake wa kuyajenga maisha yake upya umewadia. Jambo hili linaonyesha kuwa Ridhaa ana matumaini ya kuwa na maisha mazuri baadaye baada ya familia yake kuangamizwa na jirani yao Mzee Kedi.

> *Wewe, mkaza mwanangu na wajukuu wangu mmekuwa watu wa kutegemewa. Ila sasa nahisi kwamba muda wangu wa kuondoka umewadia… Noana ni muhimu nihamie ile nyumba yangu ya Afueni* (Uk. 138).

Matei anaeleza jinsi Ridhaa alivyoamua kuhamia mtaa wa Afueni. Anaeleza Mwangeka kuwa wakati wake wa kuondoka umewadia na bora aende. Kitendo hiki kinaonyesha hali ya Ridhaa kuwa na matumaini ya kuwa na maisha mazuri baada ya familia yake kuangamizwa na jirani yao. Alichukua uamuzi na kuamua kuanza maisha yake upya katika mtaa wa Afueni.

***Protagonisti katika Riwaya ya Kovu Moyoni***

Mwandishi John Habwe amebainisha mhusika Boke kuwa protagonisti katika riwaya ya *Kovu Moyoni*. Katika utafiti huu, mhusika Boke anaendeleza motifu ya mgogoro wa ardhi kwa njia nyingi. Kwanza, shamba la asili liliuzwa. Boke anakumbuka alivyouza shamba lao la nyumbani na kuhamia Rama. Alihamia Rama kwa sababu ardhi ilikuwa na rutuba nzuri ya kuendeleza kilimo. Anadai kuwa pia watu wa Rama walikuwa marafiki wakubwa. Mambo haya yalikuwa vichocheo tosha vya Boke na familia yake kuhama kwao Laka. Haya yanadhibitishwa na kifungu kifuatacho:

> *Hata alikumbuka walivyouza shamba lao la nyumbani ili kununua shamba la Rama… Watu walikuwa marafiki wakubwa. Ilikuwa nchi yenye rutuba. Ardhi ilizaa mihogo, viazi na mahindi ya ajabu* (Uk. 8).

Habwe anaonyesha jinsi mhusika Boke na mumewe walivyouza shamba lao la nyumbani. Haja yao ilikuwa kununua lingine Rama kwani watu wa Rama walikuwa marafiki na ardhi ya Rama ilikuwa na rutuba na ilizaa mimea ya ajabu. Barasa (1993) anasema kuwa chanzo cha migogoro ya ardhi ni uhaba wa ardhi yenye rotuba.

Barasa (Keshatajwa) anaeleza kuwa vita vya kikabila kuhusu ardhi huletwa na hali kwamba rasilmali huwa hazijagawa kwa usawa katika jamii. Hali ambayo huzua wivu kati ya jamii ambazo huwa hazina rasilmali dhidi ya zile ambazo zinayo. Anatoa mfano wa nchi ya Kenya ambapo Jamii ya Wakikuyu huonewa wivu na jamii zingine kwa kuwa na ardhi yenye rutuba na rasilmali nyingi kuliko jamii zingine.Kutokana na maelezo haya, ardhi yenye rotuba nzuri hupendeza wanajamii. Huwavutia watu kutamani kuishi pale. Ubora wa ardhi husaidia wanajamii kupata mazao mazuri bila kuifanyia kazi nyingi, hali inayowasaidia wanajamii kupata mavuno mengi wakipanda mimea.

Pili, mumewe aliangamizwa katika mgororo wa ardhi. Boke anafiwa na mumewe Bwana Kanja na kuachwa mjane kutokana na migogoro ya ardhi. Bwana Kanja alipigwa risasi na kuuawa na kundi la vijana lililokuwa linafurusha ‘wageni’ kutoka Rama. Risasi ilimpata alipokuwa anakimbilia usalama kujiepusha na migogoro hii. Mwandishi anasema:

> *Mwita na baba yake walikimbilia msituni. Kwa bahati mbaya risasi ikampata Kanja… Boke alipata habari za kifo cha mume wake kwa mpigo. Alipigwa risasi msituni akikimbilia usalama. Mkimbizi mama Milka, jirani yake, alimfafanulia Boke* (Uk. 10-11).

Katika gazeti la Daily Nation (October, 2021), mwakilishi wa wanawake Gatuzi la Marsabit Bi. Saffia Sheik Adan alikiri kuwa iwapo vita vya kikabila havitakomeshwa katika Gatuzi hili, wajane watazidi kuongezeka na kufanya Gatuzi hili kuwa na idadi kubwa ya wajane nchini. Hali inadhibitishwa na mwandishi anapoeleza jinsi

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1019

mumewe Boke Mzee Kanja alivyoangamizwa akitoroka Jeshi la vijana. Alipatwa risasi alipokuwa anakimbilia msituni kujinusuru.

Kutokana na maelezo haya, asasi ya ndoa huweza kuathirika pakubwa kutokana na migogoro ya ardhi. Mzazi anaweza kuangamizwa na kuacha familia na mlezi mmoja. Anayeachwa huwa na kibarua kigumu cha kukidhi mahitaji ya familia kama vile kutafuta chakula, mavazi, malazi na elimu ya watoto. Wazazi wote wakiangamia katika migogoro ya ardhi, basi watoto husalia yatima bila yeyote wa kuwahifadhi.

Tatu, kuna kukaidi ushauri wa mgogoro wa ardhi. Mhusika Boke anajuta kwa kukaidi ushauri wa Chifu Monari na kukiuza kijishamba chake cha nyumbani Laka. Chifu Monari alimsihi kutokiuza kwani hakujua Siloko alikokuwa anataka kwenda na familia yake vizuri . Boke na mumewe Bwana Kanja walikaidi ushauri wa Chifu Monari na kukiuza kishamba chao cha urithi. Mwandishi anasema:

> *"Si halali kuuza shamba lako la urithi… Hujui wendako bwana nisikize. Walisema, mtu hujua atokako sio aendako." Alisema Chifu Monari. "Hili shamba ni la mama yangu na ni letu. Tafadhali bwana Chifu usijihusishe na jambo lisilokuhusu. Hata kama litaniathiri mimi niko radhi kuathirika"* (Uk. 86).

Kwa mujibu wa Gazeti la Adili (2015), vituo vya kutoa ushauri wa kisheria hupatiana ushauri unaohusiana na masuala ya ardhi. Katika mwaka wa 2013/2014, kituo hiki kilipokea visa 3900 na visa 538 vilivyohusiana na ardhi, hali inayoupa mashiko utafiti huu. Habwe anaonyesha jinsi mhusika Boke alivyokaidi ushauri wa kutouza shamba la nyumbani. Alisema kuwa shamba hilo lilikuwa lake la kupewa na mamake. Hivyo basi, hakuhitaji ushauri wowote kulihusu.Maelezo haya yanabainisha umuhimu wa tume za kutoa ushauri kuhusiana na suala la ardhi. Tume hizi huelekeza wanajamii kuhusu mambo mbali mbali yanayohusiana na ardhi ili kupunguza migogoro yake. Wanajamii wanafaa kuusikiliza na kuufuata ushauri huu ili kuepuka migogoro ya ardhi katika jamii.

Nne, kuna mavamizi. Boke anavamiwa mara kadhaa na kundi la mashambulizi la vijana. Kundi hili lilitaka watu wote ambao si Wasuluu kurudi walikokuwa wametoka. Boke alikataa kuhama Rama na hivyo kundi hili likamvamia na kumnajisi mara kadhaa na hatimaye kupata ugonjwa wa nasuri. Mwandishi anasema:

> *Lakini hivi ndivyo ilivyokuwa. Walimnajisi Boke akabaki hali hoi. Hasemi, hasogei. Ni kama aliyekufa. Maana ameonywa mara nyingi kuondoka, ameshambuliwa mara nyingi lakini hasikilizi* (Uk. 43).

Aidha, ubakaji unampelekea Boke kupata ungojwa wa nasuri kutokana na vitendo vya kinyama anavyofanyiwa na Jeshi la vijana. Mwandishi anasema:

> *"Mamako ana nasuri. Kitendo cha kihayawani alichotendewa ndicho kilichomsababishia hali hiyo," Nesi alimweleza …Hapo ndipo Eddah alipomweleza Nesi pia hata yeye aliathirika na hivyo vitendo vya kinyama* (Uk. 44).

Wanawake wa Kihindi kutoka Gatuzi la Lamu wameitisha kitendo cha haraka kuhusiana na mavamizi wanayovamiwa kuhusu migogoro ya ardhi (Chome,2020). Wanakiri kuwa Lamu imeshuhudia visa vingi vya mavamizi vinavyohusiana na ardhi baina ya wanajamii. Hali hii inabainishwa na mwandishi anapoonyesha mhusika Boke alivyobakwa na kubakia hoi kwa kukaidi kuondoka pale Rama.

Tano, kuna mashambulizi. Boke ameshambuliwa mara kadhaa. Kitendo kinachompelekea kupata ugonjwa wa nasuri. Nesi alimwambia mwanawe Eddah kuwa mama yake ana ugonjwa wa nasuri kutokana na vitendo vya kinyama alivyofanyiwa na Jeshi hilo. Maelezo haya yanabainisha kuwa panapozuka migogoro ya ardhi, wanajamii huathirika sio tu kisaikolojia bali hata kiafya wanapopata magonjwa mbali mbali.

Sita, kuna kushikwa mateka. Jeshi la vijana linamshika mwanawe Boke mateka. Mwita alishikwa na Jeshi la taifa lililodai kuwa yeye ni mmoja wa wanajeshi la vijana. Kitendo hiki cha kusingiziwa kinamfanya Mwita kukosa tamaa ya kuwa huru maishani. Alipopelekwa mahakamani, Mwita alikataa kujibu mashtaka na hivyo jaji akaamua anyongwe.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1019

> *King'ora kililia mara tatu ishara ya kwamba Mwita alikuwa amenyongwa tayari. Mama yake alipewa nguo zake akaondoka ...* (Uk. 132).

Watoto katika maeneo yaliojaa migogoro ya ardhi hususani Barani Afrika huwa wengi. Baadhi ya watoto hawa hugeuka kuwa wanajeshi. Imekadiriwa kuwa hawa wanajeshi wadogo ni takribani 300,000 na wamo kati ya umri wa miaka 10 na 24. Baadhi ya hawa watoto huwa wamelazimishwa kujiunga na vikundi hivi. Hali inabainishwa na mwandishi anapoonyesha Mwita, mwanawe Boke alivyoshikwa mateka na Jeshi la Vijana. Aidha, alishikwa na jeshi la taifa lilipodai kuwa yeye ni mmoja wa jeshi la vijana.Kutokana na maelezo haya, watoto wanaweza kutumiwa vibaya na kulazimishwa kufanya mambo yatakayowadhuru baadaye. Mifano ya mambo haya ni pamoja na kuingizwa katika vikundi haramu katika jamii vinavyozua migogoro ya ardhi katika jamii.

Sita, kuna shamba lililonunuliwa. Boke na mmewe Mzee Kanja, wanaamua kununua shamba Rama. Wazo lao la kununua shamba Rama ni kwa sababu Rama ardhi ilikuwa na rutuba nzuri ya kuendeleza kilimo. Rotuba ilivutia wakulima wengi kwani baada ya kulima walipata mavuno mengi. Mwandishi anasema:

> *Siloko mlimani ni mahali palipozungukwa na mito miwili. Ardhi yake ina rutuba nyingi. Mimea ilimea bila kutiwa mbolea. Ni mahali palipovuta tamaa ya watu. Kila aliyepaingia aliona taabu kupatoka* (Uk. 86).

Habwe anaonyesha sababu kuu ya mhusika Boke kuhama kwao Laka na kununua shamba Siloko ni kuwa ardhi ilikuwa na rutuba nzuri ya kuendeleza kilimo. Hali ya rutuba nzuri ilipelekea watu wengi akiwemo Boke kutotaka kuhama Siloko. Utafiti huu ulibainisha kuwa ardhi yenye rutuba huvutia idadi kubwa ya watu kuipenda na kutamani kuitumia kwa kueneza kilimo kama wanavyofafanua waandishi wa riwaya teule.

**Wahusika Antagonisti**

Antagonisti ni wahusika wanaojulikana kuwa wabaya katika kazi za fasihi kwa sababu hupigana na protagonisti ili kuzuia mafanikio ya kupata wanachotaka kukipata (Saraswati, 2019). Kwa kawaida, huwa ni wahusika duara wanaobadilika kutegemea hali na wakati wa matukio ya kifasihi. Ni wahusika ambao ni lazima protagonisti wapigane nao ili wapate ushindi. Hata hivyo, Wahusika antagonisti si lazima wawe watu bali inaweza kuwa hali inayojenga kizingiti kwenye njia ya protagonisti ili asifanikiwe kufikia shabaha yake katika kazi ya fasihi (Zengin, 2015). Matei, mwandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri* amebainisha mhusika Lunga Kiriri Kangata kuwa antagonisti. Lunga anakuza motifu ya mgogoro wa ardhi kupitia njia nyingi.

Kwanza, kuna kuwa mlowezi katika Msitu wa Mamba. Lunga anakuwa mlowezi katika msitu wa Mamba. Kutokana na faida anayopata kutokana na mazao ya kilimo anachoendeleza katika msitu anakosa hamu ya kurudi kwao katika awamu ya pili ya Operesheni Rudi Edeni. Anakita katika msitu huu hadi pale uongozi unaamua kumtimua kwa nguvu pamoja na familia yake.

> *Wachache walifanikiwa kurudi kwao katika awamu ya pili ya Operesheni Rudi Edeni. Wengine kama Lunga, ambaye tangu hapo hakujua kitovu chake hasa, walitimuliwa pamoja na familia zao* (*Chozi la Heri*, Uk. 76).

Hakuna pingamizi kuwa ardhi ni chombo muhimu cha uzalishaji mali katika maisha ya binadamu. Ni vigumu kupata kazi yeyote ya kuendeleza uchumi inayoweza kuendelezwa bila kuhusisha ardhi, hivyo basi, kuonyesha umuhimu wa ardhi (Gambrah, 2002). Hali hii inabainishwa na Matei anaposema kuwa ni wakimbizi wachache waliofanikiwa kurudi kwao katika awamu ya pili ya Operesheni Rudi Edeni. Hata hivyo wengine kama Lunga ambao hata hawakujua asili yao, walitimuliwa pamoja na familia zao.

Kutokana na maelezo haya, ardhi ni rasilmali muhimu sana katika jamii yoyote, jambo linalowapa waja hamu ya kutamani kuishi sehemu fulani. Hali hii hueleza kwa nini sehemu fulani za jamii huwa na idadi kubwa ya watu kuliko zingine.

Pili, kuna kumiliki ardhi kubwa. Lunga anamiliki ardhi kubwa ya ekari thelathini na tano katika msitu wa Mamba ambapo anaendelezea kilimo. Lunga alipofutwa kazi alirithi shamba kubwa aliokuwa nalo babake katika msitu wa Mamba. Aliendeleza kilimo kwa lengo la kuuza na kupata faida. Mwandishi anasema:

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1019

> *Mara tu macho yake yalipokumbana ana kwa ana na zao la mahindi lililotamalaki kwa heba katika ekari thelathini na tano ambazo zilikuwa milki ya baba yake, moyo wa Lunga ulitwaa uchu …Alipanda mimea zaidi kwa ajili ya kuuza* (*Chozi la Heri*, Uk. 73)

Joan (2013) aliangazia swala la unyakuzi wa ardhi na athari yake kwa chakula katika jamii ya Senegal. Utafiti wake ulidai kuwa taifa la Senegal huchangia kuharakisha 'unyakuzi wa ardhi' hali inayochangia kuhatarisha hali ya chakula katika jamii hii. Matei anatilia madai haya mashiko anapoonyesha jinsi mhusika Lunga alivyonyakuwa ardhi kubwa ya ekari thelathini na tano katika msitu wa Mamba. Uchu wa kuendeleza kilimo kwa lengo la kuuza ulimfanya kunyakua ardhi ya msitu zaidi.

***Antagonisti katika Riwaya ya Kovu Moyoni***

Katika riwaya ya *Kovu Moyoni*, wahusika antagonisti ni Kundi la Jeshi la Vijana. Kundi hili linakuza motifu ya mgogoro wa ardhi kupitia hali nyingi. Kwanza,kuna kufurusha wageni wote. Jeshi la vijana linadai kuwafurusha wageni wote Rama. Dai lao kuu ni kwamba wageni walikuja na kuuziwa mashamba Rama ambayo yalistahili kuwa yao. Wanadai kuwa mashamba yote ambayo wageni waliuziwa ni kupitia kwa ufisadi wa kughushi hatimiliki za ardhi hizo.

> *Vijana hao walikutana katika vikundi vidogo vidogo na wakaanzisha siasa Fulani. Siasa za kunyakua ardhi ambayo walidai kuwa ilikuwa ni yao na iligawanywa vibaya kwa kupitia kwenye msingi ghushi. Wazo hili hatari lilichipuka kupitia miongoni mwa vijana wa Kisululu waliodhania kuwa ndilo kabila asilia la sehemu hiyo* (Uk. 15).

Tofauti za kikabila ni miongoni mwa vyanzo vikubwa vya migogoro ya ardhi. Machafuko katika sehemu mbalimbali duniani hususani barani la Afrika huchochewa na ukabila. Mwandishi anashadidi anapoonyesha Kundi la vijana likibuni kikundi maalumu cha kuwafurusha wageni wote kutoka Rama. Linadai kuwa Kabila la Wasuluu ndilo kabila asili na makabila mengine yote yanapaswa kuondoka Rama. Kutokana na dhibitisho hili, tofauti za kikabila huzua migogoro ya ardhi miongoni mwa mwanajamii. Serikali kuu na za magatuzi zinapaswa kuhakikisha kuwa zimeunda sera madhubuti zitakazouzima ukabila katika jamii, jambo litakaloendelaza jamii tulivu itakayoweza kufikia malengo yake.

Pili,  kuna kuchoma mimea. Jeshi linachoma stoo, mifugo na shamba la ngano la Chifu Ngata. Jeshi linatekeleza kitendo hiki baada ya kumvamia na kumuua Chifu Ngata. Vijana hawa walidai kuwa Chifu Ngata alikuwa kati ya 'wageni' waliostahili kufurushwa Rama.

> *Walipokuwa wanaomboleza kifo cha baba yao na jamaa, ndimi za mashambulizi ziliwaka hata zaidi. Washambulizi walirudi tena wakachoma stoo, mifugo, shamba la ngano na nyumba kubwa* (*Kovu Moyoni*, Uk. 51).

Kwa mujibu wa Nyiri (2014), sekta ya kilimo nchini Kenya ilipata hasara kubwa haswa kwa wakulima wa majani chai na maua wanaouza Ulaya. Anafafanua pia wakulima wa Maua (Nakuru) na majani chai (Kericho) walipata hasara kubwa baada ya mimea hii kuchomwa katika machafuko ya baada ya uchaguzi. Habwe anadhibitisha hili anapoonyesha jinsi kundi la Jeshi la Vijana lilivyomvamia Chifu Ngata. Baada ya kifo chake, jeshi hili lilirudi tena na kuchoma stoo, mifugo, shamba la ngano na nyumba kubwa.

Tatu, kuna kuunda kikundi maalumu cha kulinda ardhi. Jeshi la vijana linaunda kikundi maalum kinachojumuisha vijana wasiokuwa na kazi katika Rama. Kundi hili lilikuwa na lengo moja kuu la kuwafurusha wageni wote ambao hawakuwa Wasuluu katika jamii yao. Jeshi lilikuwa na kiongozi wao aliyeitwa Meja.

> *Kwa ajili ya ukakamavu wake, alifanywa kiongozi wa kikundi hicho… Meja-K alijifunga njuga za ukombozi akaingia uwanjani kwa ushindani. Meja-K ambaye awali alikuwa mtulivu kama njiwa akawa mkali kama nyati* (*Kovu Moyoni*, Uk. 18).

Kikundi cha Al-Shabaab nchini Somali huzuia wakimbizi Somali kupata chakula cha msaada wala wao kuondoka na kwenda kutafuta usaidizi kwingine. Kikundi kimefanya wakimbizi wa ndani nchini Somalia kuongezeka mno. Al-Shabaab hudhibiti Somali ya Kusini na huwa na muungano na kikundi haramu duniani cha Al-qaeda (Sarah, 2011). Habwe anadhibitisha haya kwa kuonyesha

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1019

jinsi vijana Rama waliunda kundi walilodai lilikuwa la kulinda ardhi yao. Kundi hili lilikuwa na kiongozi aliyeitwa Meja-K. Kiongozi huyu alichaguliwa kutokana na ukakamavu wake. Yeye ndiye aliyeongoza shughuli zote za kundi hili. Mwandishi anasema:

> *Meja-K, akiwa amevaa sare ya kijani ya Amiri Jeshi, alikagua vyombo hivyo… Meja-K alienda kuikagua gwaride na kuihutubia* (*Kovu Moyoni*, Uk. 27).

Kutokana na dhibitisho hili, ardhi ni nyenzo muhimu katika jamii. Umuhimu wake huchangia wanajamii kujipa uwezo wa kuweza kudhibiti. Hali ambayo huzaa makundi haramu ambayo huleta machafuko ya ardhi katika jamii.

Aliyekuwa Waziri wa Elimu Amina Mohammed nchini Kenya akitangaza matokeo ya mtihani wa kitaifa wa darasa la nane desemba mwaka wa 2018, alisema kuwa kuna baadhi ya shule ambazo matokeo yao hayakutolewa kwani yanachunguzwa kufuatia wizi wa mtihani huo. Waziri huyu alisema kuwa hatua hii itakuwa changamoto kwa serikali na mashirika ya nje kwani baadhi ya wanafunzi hao watajiunga na makundi haramu duniani (Daily Nation, 31 Desemba, 2018). Habwe anatilia hili mkazo anapoonyesha waliokuwa wanasoma na Nifreda na Mwita lakini sasa wamejiunga na Kundi la Vijana linalowashambulia Boke na Chifu Ngata baba yake Nifreda.

Kutokana na dhibitisho hili, vijana ni chombo kinachoweza kutumiwa kuharibu mazingira haswa wasipopewa mwongozo na msingi dhabiti wa kielimu. Hivyo basi, serikali inapaswa kuweka sera madhubuti katika Wizara ya Elimu ya kuhakikisha kuwa vijana wote wamepata elimu haswa ya kutunza mazingira.

### *Wahusika Bui katika Riwaya ya Chozi la Heri*

Wahusika bui ni wandani wa mhusika mkuu na kupitia kwa ufichuaji wa siri baina yao sifa za mhusika mkuu huwekwa wazi (Saraswati, 2019). Ilibainika kuwa mhusika Tila ni bui katika riwaya ya *Chozi la Heri*. Tila anakuza motifu ya mgogoro wa ardhi kwa njia nyingi. Kwanza, kuna Kufafanua hali ya ardhi katika sehemu kame. Tila anakuza motifu ya mgogoro wa ardhi anapomweleza baba yake kuwa ni watu wengi wanaoishi katika sehemu kame na ambao hawapati chakula cha kutosha kwani ardhi haiwezi kustahimili mimea yeyote. Watu hao pia hawawezi kumudu chakula cha kuwatosha kwa siku.

> *Baba, wewe mwenyewe unalalamika kiangazi ambacho kimezikumba sehemu mbali mbali nchini. Isitoshe, Mwalimu asema kwamba asilimia kubwa ya wakazi wa sehemu kame haiwezi hata kumudu kula mara mbili kwa siku* (*Chozi la Heri*, Uk. 43).

Sehemu kame huchukua zaidi ya asilimia arobaini ya sehemu ya ardhi. Kilimo katika sehemu hizi hulemazwa na vigezo kama vile maji, joto kali, mvua kutotosha, upepo mkali na udongo kavu (Golla ,2021). Tila anamweleza baba yake kwamba mwalimu wao alisema kwamba asilimia kubwa ya wakazi wa sehemu kame haiwezi hata kumudu kula mara mbili kwa siku.

Kutokana na maelezo haya, ardhi katika sehemu kame haiwezi kustahimili mimea yoyote. Hii ndio maana watu wanaoishi pale hukosa chakula, hali inayofanya sehemu hizi kutegemea chakula cha msaada kutoka kwa serikali au mashirika yasiyo ya kiserikali.

Pili, kuna umaskini. Tila anabainisha umaskini unaowakumba wanajamii hivi kwamba hawawezi kumudu kuvumbua mbinu za kuyahifadhi maji ya mvua. Anamweleza baba yake kuwa wanajamii hawana hela za kununulia matangi ya kuhifadhi maji.

> *Mathalan, watu wanaoishi katika sehemu kame wanastahili kujitahidi kuvumbua mbinu za kuyahifadhi maji ya mvua… Hizo hela za kununulia matangi ya kuhifadhia maji na kufanyia utafiti watazitoa wapi*? (*Chozi la Heri*, Uk. 43).

Tatu, kuna kuonyesha umuhimu wa ardhi. Tila anaonyesha umuhimu wa ardhi kwa kufafanua kuwa ardhi ni tegemeo la wanajamii wengi. Baadhi ya watu wamekuwa wategemezi wa mvua, hali inayowapelekea kukosa chakula mvua inapokosa kunyesha. Hali hii huzua jamii yenye njaa na kuzuka kwa magojwa yasababishwayo na njaa. Assumpta anasema:

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1019

> *Watu wengi huko mashambani hutegemea mashamba, mvua haijakubali kunyesha kwa muda. Wengi wa wanaofanya kazi za ajira, hufanya kazi za kijungu jiko* (Uk. 43).

Wakulima wengi nchini India hutegemea mvua kuendeleza kilimo. Hii ni kwa sababu kilimo ni mojawapo ya vyombo muhimu vya kuendeleza uchumi wa India (Karnawat na wengine ,2020).Hii ndio maana Assumpta anarejelea mhusika Tila akionyesha jinsi wanajamii haswa wanaoishi mashambani hutegemea mvua ili kuweza kuendeleza kilimo.

Maelezo haya yanatupa picha ya utegemezi wa wakulima kwa mvua. Wizara ya Kilimo inapaswa kuwapa wakulima mafunzo tosha ya mbinu badala wanazoweza kutumia ili kupata maji ya kuendeleza kilimo. Huu utakuwa mchango mkubwa wa kuinua uchumi wa mataifa mengi.

**Wahusika Bui katika Riwaya ya *Kovu Moyoni***

Katika Riwaya ya *Kovu Moyoni* mhusika bui ni Emoro. Anakuza motifu ya ardhi kupitia njia nyingi. Kwanza, kuna kuuawa. Emoro anauawa katika kijishamba cha miwa kwa kuonwa kuwa mgeni Rama. Boke anakumbuka jinsi Emoro alivyofukuzwa na kuingia katika kijishamba cha miwa na wafuasi wake kumfuata na kumchoma hadi kifo kwani alikuwa mmoja kati ya 'wageni' waliokuwa wanafukuzwa Rama.

> *Alikumbuka jinsi jirani yake Emoro alivyofukuzwa akaingia ndani ya shamba la miwa. Watesi wake walimfuata na kumchomea humo shambani. Hadi hivi leo Boke hukumbuka sauti ya Emoro ikiomba msaada wa kuokolewa* (*Kovu Moyoni*, Uk. 2).

Makunike (2014), alichunguza mabadiliko ya ardhi na hali ya umaskini Zimbabwe. Utafiti wake ulibainisha kuwa, katika Mashonaland wakulima walikuwa wanatukanwa, kuteswa na hatimaye kuuawa. Habwe anatilia haya mkazo anapoonyesha mhusika Emoro alivyouawa akijaribu kutoroka kunusuru maisha yake baada ya migogoro ya ardhi. Aliuawa kwa kushukiwa kuw a ni 'mgeni' pale.Kutokana na dhibitisho hili, suala la ardhi huleta chuki katika jamii. Chuki hii hatimaye huzaa ukabila unaokuza ubaguzi katika jamii. Serikali inapaswa kukemea hali hii kwa vyovyote vile ili kuepuka machafuko ya kikabila yaletwayo na migogoro ya ardhi.

Pili, kuna kuhama. Emoro anahama kutoka kwao kwa sababu hakupata shamba la kuridhi kutoka kwa wazazi wake. Baba yake alikuwa na wake watano naye mama yake aliaga akiwa bado mtoto. Hakuweza kuvumilia mamaye wa kambo na hivyo akaamua kuhama. Mwandishi anasema:

> *Aliwaeleza Boke na mzee kuwa baba yake alikuwa na wake watano. Yeye Emoro, akawa hajabahatika kupata chochote kwa baba yake. Mamake alifariki yeye alipokuwa mdogo… hakuweza kuvumilia vitimbi vya mama zake wa kambo* (Uk. 3).

Castelli (2018), anafafanua kuwa baadhi ya vichocheo vya watu kuhama ni masomo, dini na uamuzi wa mtu binafsi. Mawazo haya yanashadidiwa na Habwe anapoonyesha mhusika Emoro akihama kwao kwa sababu ya wao kuwa wengi na kukosa chochote cha kurithi kutoka kwa wazazi. Kutokana na maelezo haya, ukosefu wa ardhi unaweza kufanya mtu kuhama kutoka sehemu moja hadi nyingine. Hii inaeleza kwa nini baadhi ya watu hutoka walikozaliwa na kuishi kwingine.

Tatu, kuna kununua shamba. Emoro ananunua shamba la robo ekari Muhoroni. Hapo Muhoroni aliibuka mkulima hodari kwa kulima mimea mbali mbali kama vile vitunguu, viazi mbatata, viazi vitamu, kabichi na karoti na kuwaulizia watu. Mwandishi anasema:

> *Aliamua kununua shamba Muhoroni la robo ekari. Humo shambani alipanda vitunguu, viazi mbatata, viazi tamu, kabichi na karoti* (*Kovu Moyoni*, Uk. 3).

Ardhi humpa mtu utulivu wa akili. Haiwezi kuibiwa wala kuharibiwa. Ardhi tu vile ilivyo itakuwa na manufaa makubwa (Ryan,2021). Hali hii inatiliwa mashiko naye Habwe anapoonyesha mhusika Emoro akiamua kununua kipande cha ardhi Muhoroni. Humo shambani aliendeleza kilimo kwa kupanda mimea.

Maelezo haya yanaonyesha kuwa ardhi inaweza kutumiwa kuendeleza kilimo. Mimea kama vile karoti, kabichi, na viazi tamu vinaweza kupandwa na kufanya vizuri. Emoro anajituma kufanyia watu

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1019

kazi shambani. Alipohamia Rama, alilimia watu na kuwapandia viazi wakati wa msimu wa upanzi. Hali iliyomfanya kupendwa na watu wengi aliowafanyia kazi hii.

> *Alilimia watu na kuwapandia viazi wakati wa msimu wa upanzi. Lile jina la Mkulima la kule Muhoroni likamrudia tena* (*Kovu Moyoni*, Uk. 4).

Watu bilioni 1.1 hufanya kazi ya kilimo. Hii inajumuisha kadri ya watu kati ya milioni 300-500 kama wafanyakazi na ambao hutegemea malipo yao kutoka kwa kilimo. Sekta hii vile vile ina vibarua wengi ambao hufanyia wakulima wadogo wadogo kazi. Habwe anadhibitisha haya kupitia kwa mhusika Emoro ambaye alifanyia watu kazi ya kuwapandia viazi wakati wa msimu wa upanzi.Kutoka na maelezo haya, ardhi inaweza kuwa tegemeo la jamii haswa kwa chakula na fedha. Wanajamii wanapaswa kuwa na motisha ya kufanya kazi ili kuinua viwango vya mapato shambani kama wakulima, wafanyakazi au vibarua shambani.

Nne, kuna kufukuzwa. Emoro anafukuzwa Rama kuwa yeye ni mgeni. Jeshi la vijana liliwafukuza wageni wote waliokuwa Rama. Emoro aliwaomba msamaha lakini hawakumsikia na hatimaye wakamchoma na akafa. Mwandishi anesema:

> *"Msiniue! Niko tayari kuliacha shamba hilo nirudi kwetu. Niachieni roho yangu! Nyinyi ni ndugu zangu! Nawaomba! Ninawasihi!"* (*Chozi la Heri*, Uk. 2).

Katika jamii nyingi za Kenya, ni vigumu kutenganisha ardhi na watu. Hii ni kutokana na mshikamano mkubwa uliopo baini ya ardhi na wanajamii wanaoimiliki. Hali hii ndio huzua migogoro ya ardhi wakati wenyeji hushindwa kuachilia ardhi hii kwa wageni wakishainunua. Hali hii iliibuka nchini Kenya wakati wa uchaguzi mkuu wa 2007. Habwe anabainisha haya kupitia kwa mhusika Emoro alipotimuliwa kwa kuonwa kuwa mgeni na Kundi la Jeshi la Vijana. Kutokana na maelezo haya, suala la ardhi linaweza kuleta machafuko katika jamii. wanajamii wanapaswa kutumia njia zingine katika kusuluhisha migogoro ya ardhi na wala sio vita.

## HITIMISHO

Lengo la Makala hii lilikuwa kuchunguza jinsi wahusika walivyofanikisha ujenzi wa motifu ya mgogoro wa ardhi katika riwaya ya *Chozi la Heri* na *Kovu Moyoni*. Ilibainika kuwa Katika riwaya ya *Chozi la Heri*, mhusika Ridhaa ni protagonsti. Ridhaa ameonyesha kuwa suala la mgogoro wa ardhi linaweza kufanya nyumba kuchomwa, kubomolewa, kutolewa ushauri, kushirikishwa katika mijadala, kujengewa mabomba ya maji na kufanya mtu kuhama na kwenda kuishi sehemu nyingine.Katika riwaya ya *Chozi la Heri* mhusika Boke ni protagonisti. Amebainisha kuwa suala la mgogoro wa ardhi linaweza kufanya mja kuuza shamba lake la asili, mumewe kuangamizwa, kukaidi ushauri wa suala la ardhi, kufanya mtu kuvamiwa na kununua shamba maeneo mengine.

Waandishi wa riwaya teule wamebainisha wahusika antagonisti kuwa Lunga katika riwaya ya *Chozi la Heri* Jeshi la Vijana katika riwaya ya *Kovu Moyoni*. Lunga ameonyesha kuwa suala la mgogoro wa ardhi linaweza kuleta kukata miti, walowezi, tamaa ya kumiliki ardhi na kubadilisha mtazamo wa ardhi. Kundi la Jeshi la vijana limebainisha mgogoro wa ardhi kwa kuwafurusha wageni, kuchoma mimea, kuunda kikundi cha kulinda ardhi na kuharibu mali.

Wahusika bui ni Tila katika riwaya ya Chozi na Emoro katika riwaya ya Kovu Moyoni.Tila amebainisha suala la mgogoro wa ardhi kwa kufafanua hali ya ardhi,kuonyesha umaskini na kuonyesha umuhimu wa ardhi.Naye Emoro amebainisha suala la mgogoro wa ardhi kwa kuuawa,kuhama ,kununua shamba na kufukuzwa.

## MAREJELEO

Barasa, N. (1993). Of Ethnicity and Leadership in Kenya. *The Daily Nation, 3rd April, Nairobi*.

Castelli, F. (2018). Drivers of migration: why do people move?. *Journal of travel medicine*, *25*(1), tay040.

Chome, N. (2020). Land, livelihoods and belonging: negotiating change and anticipating LAPSSET in Kenya's Lamu county. *Journal of Eastern African Studies*, *14*(2), 310-331.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1019

Cuddon, A. (2013). A Dictionary of Literary Terms and Literary Theory. Wiley: Blackwel

Ertiftik, H., & Zengin, M. (2015). Effects of increasing rates of potassium and magnesium fertilizers on the nutrient contents of sunflower leaf. *Selcuk Journal of Agriculture and Food Sciences*, *29*(2).

Gambrah, A. (2002), "Improving Land Transfer Procedures in Ghana", Journal of Kwame Nkrumah University of Science and Technology, Kumasi, Vol. 22, pp. 22-24.

García, N. (2016). Moral emotions, antiheroes and the limits of allegiance. In *Emotions in contemporary TV series* (pp. 52-70). Palgrave Macmillan, London.Global land programme.

Golla, B. (2021). Agricultural production system in arid and semi-arid regions. *International Journal of Agricultural Science and Food Technology*, *7*, 234-244.

Gyamera, E., Duncan, E. E., Kuma, J. S. Y., & Arko-Adjei, A. (2018). Land acquisition in Ghana; Dealing with the challenges and the way forward. *Journal of Agricultural Economics, Extension and Rural Development*, *6*(1), 664-672.

Habwe, J. (2014). *Kovu Moyoni*. Bookmark Africa.

Karnawat, M., Trivedi, S. K., Nagar, R., & Nagar, D. (2020). Role of monsoon in Indian agriculture. *Biotica Research Today*, *2*(10), 1019-1021.

LaFrancesca, Joanna. "Land grabs and implications on food sovereignty and social justice in Senegal." (2013).

Makunike, B. (2014). *Land reform and poverty alleviation in Mashonaland East, Zimbabwe* (Doctoral dissertation, University of the Free State).

Matei. K. (2017) *Chozi la Heri*. One Planent & Media Services Limited.

Morgan, D. O. (1995). Principles of CDK regulation. *Nature*, *374*(6518), 131-134.

Mugenda, O. M., & Mugenda, A. G. (1999). *Research methods: Quantitative and qualitative approaches*. Acts press.

Mulokozi, M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili.* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili: Dar es Salaam.

Nyiri, K. (2014). The impact of ethnic conflict on economic development: the case of post-election violence in Kenya, 2007-2014 (Doctoral dissertation, University of Nairobi).

Ryan-Collins, J. (2021). Breaking the housing–finance cycle: Macroeconomic policy reforms for more affordable homes. *Environment and Planning A: Economy and Space*, *53*(3), 480-502.

Sarah. S. (2011) AL-Shabaab makes it hard for internally displaced Somalis to access aid-One

Saraswati, K. P. (2019). Analysis of Characters and Characterization in the Compilation of Malay Poetry "Mirror. Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Negeri Semarang.

Scott, G. (2015). *Migogoro ya Kisaikolojia katika Riwaya ya Mkamandume na Unaitwa Nani*. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.

Taifa la Kenya. (2010). *Katiba ya Kenya*. Nairobi: Government Printer.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki WA fasihi*.

Wamitila, W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*, Nairobi; Focus Publication Ltd.

Wien, N. R. (1916). Karl Marx und Friedrich Engels über die Polenfrage. *Archiv für die Geschichte des Sozialismus und der Arbeiterbewegung*, (6), 175.

Wizara ya Ardhi, (2009). *Sessional paper No.3 of 2009*. Nairobi: Government Printers.

Zhang, K., Yu, Z., Li, X., Zhou, W., & Zhang, D. (2007). Land use change and land degradation in China from 1991 to 2001. *Land Degradation & Development*, *18*(2), 209-219.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.